# Mambo 9 yanayowezesha ukuaji wa bluu kwa wenyeji katika nchi zinazoendelea

Muhtasari wa sera kutokana na tafiti nne za usuli



Ripoti 2022:11

Swedish Agency for Marine and Water Management

# Waandishi

Maria Göthberg, Gonçalo Carneiro,
Linus Hammar, Wilhelm Gårdmark,
Ingela Isaksson

# Yaliyomo

Mambo 9 yanayowezesha ukuzi wa bluu kwa wenyeji katika nchi zinazoendelea ..............3

1. Miundombinu ya kutosha, inayoweza kufikiwa na iliyotunzwa vizuri ni hitaji kuu kwa ukuaji wa bluu kwa wenyeji .3
2. Upatikanaji wa mikopo huruhusu uwekezaji mpya, uboreshaji wa kiufundi na huongeza ustahimilivu.....4
3. Kuandaa na kupanga washiriki wenyeji huchangia ukuaji wa Bluu .....4
4. Mifumo na sera zinazopatana na zinazotabirika huunda msingi wa kujenga ukuaji wa bluu kwa wenyeji .5
5. Kanuni za mazingira zilizopatanishwa na hali na zinazoeleweka vizuri hudumisha ukuaji wa bluu......................5
6. Ujumuishaji pamoja na hatua zinazoongeza thamani na inayofanya kazi vizuri ni muhimu kwa kuendeleza uchumi wa bluu kwa wenyeji ................6
7. Usimamizi bora wa taasisi zinazofanya kazi ni msingi wa ukuaji wa bluu kwa wenyeji.................................6
8. Ubunifu huchochea teknolojia iliyoboreshwa na michakato bora zaidi wa uchumi wa bluu kwa wananchi ........................................................7
9. Mpangilio wa kimkakati unasaidia kuondoa vizuizi na kutayarisha njia kwa ajili ya ukuaji wa bluu kwa wenyeji .............................................................7

Jinsi tulivyofanya: tafiti nne ndani ya moja ........8

Mifumo ya ikolojia inayofanya kazi ni muhimu .8

Marejeleo...........................................................................9

Kuhusu sisi ....................................................................... 11

Muthasari huu wa sera umetolewa na Wakala wa Uswidi wa Usimamizi wa Bahari na Maji. Wakala unawajibika kwa ajili ya yaliyomo na hitimisho la muthasari wa sera.

© Swedish Agency for Marine and Water Management | Tarehe: 2023-10-17

ISBN: 978-91-89329-40-9

Michoro: © Swedish Agency for Marine and Water Management (CC BY-SA) | Where is my pony whereismypony.se

Swedish Agency for Marine and Water Management | Box 11 930 | 404 39 Gothenburg | www.havochvatten.se/en

# Mambo 9 yanayowezesha ukuaji wa bluu kwa wenyeji katika nchi zinazoendelea

Muhtasari huu wa sera unawasilisha **mambo tisa muhimu ya kitaasisi na miundombinu** yanayochangia **ukuaji wa bluu kwa wenyeji** kutokana na matumizi ya rasilimali za baharini katika nchi zinazoendelea.

Muhtasari wa sera umetolewa na Wakala wa Uswidi wa Usimamizi wa Bahari na Maji, na unategemea tafiti nne za usuli, zote zikishughulikia swali moja: ni nini kinachohitajika ili rasilimali za baharini zizalishe ukuaji wa bluu kwa wenyeji.

Hapa, ukuaji wa bluu kwa wenyeji unarejelea mapato ya kiuchumi na ustawi katika jamii ya wenyeji kutokana na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, kama vile uvuvi, ufugaji wa samaki, au utalii.

## 1. Miundombinu ya kutosha, inayofikika na iliyotunzwa vizuri ni hitaji kuu kwa ukuaji wa bluu kwa wenyeji.

Biashara za bluu zinategemea miundombinu inayofikika, inayotegemeka na iliyo bora. Hii inatia ndani **miundombinu ya msingi** kama vile barabara nzuri, umeme, maji ya kunywa, usafi na mawasiliano ya simu, na vile vile **miundombinu maalum ya bahari** kama bandari, maeneo ya kutua, vifaa vya matengenezo vinavyopatikana karibu, ghala la kuhifadhi baridi na vifaa vya usindikaji.

Bila kujali kama miundombinu kama hiyo inatolewa na taasisi za umma au za kibinafsi, **upatikanaji wake unahusiana** sana na **ustawi** wa kijamii na kiuchumi katika miktadha mingi.





Kwa ujumla, upatikanaji wa miundombinu ya msingi na ya baharini ni **takwa** la kuwezesha **uwekezaji** katika uchumi wa bluu.

Ni muhimu kwamba miundombinu **itunzwe vyema**, ili iendelee kufanya kazi kwa muda mrefu iwezekanavyo. Mazingira ya baharini ni kali sana kwa vifaa vya kiufundi, hivyo matengenezo siku hadi siku ni muhimu katika sekta yoyote ya bluu.

Uwekezaji wa miundombinu unahitaji **kuzingatia athari mbaya zisizotarajiwa**, hasa kwa masuala ya matokeo mabaya ya mazingira na kijamii, hasa kwa jamii zilizo hatarini kuahiriwa vibaya.

## 2. Upatikanaji wa mikopo huruhusu uwekezaji mpya, uboreshaji wa kiufundi na huongeza ustahimilifu

**Upatikanaji** ulioboreshwa **mkopo** huongeza fursa kwa wanajamii na mashirika kutokeza ukuaji wa bluu. Mifano ya hatua hizo ni kutoa dhamana ya fedha za umma ili kunga mikono mikopo ya kibinafsi, kuweka hatua za misaada ya dharura ili kuepusha hatari za mazingira na kutoa mikopo ya umma kwa uwekezaji katika vifaa vya uzalishaji na taasisi za mikopo midogo midogo.

Changamoto moja ni jinsi taasisi za mikopo mara nyingi zinavyopendelea wale ambao tayari wana bafa, kwa mfano kwa **kudai dhamana** kwa ajili ya kutoa mikopo au kuweka **mipango ya ulipaji** inayobana sana. Hii inaweza kuwa changamoto kwa biashara nyingi ndogo ndogo, kwani mara nyingi hazina rasilimali za kutosha za kifedha au nyenzo, na zinahitaji muda zaidi kabla ya




kupata mapato ya kutosha na kushinda udhaifu unaokuwepo mwanzoni.

Upatikanaji wa **mikopo kwa biashara ndogo** unaweza kufungua fursa kwa wanajamii na mashirika kuanzisha biashara mpya, kuboresha biashara zilizopo tayari na kuimarisha uwezo wao wa kukabiliana na hali ngumu na gharama zisizotarajiwa.

## 3. Kuandaa na kupanga washiriki wenyeji huchangia ukuaji wa bluu

**Mashirika ya kijamii** na **mitandao** yana majukumu muhimu kwa ajili ya maendeleo kwa wenyeji. Kuwa mwanachama kunaweza kuongeza mapato na fursa za ajira ya uvuvi, ufugaji wa samaki, na utalii.

Mashirika haya yanahitaji **uongozi halali na mahiri**. Wanapaswa kuhimiza wahusika wote watumie kanuni na maadili yaleyale, pamoja na kutoa mafunzo ya kiufundi na kuongeza uwezo.

**Usimamizi unaotegemeka** ni muhimu pia kwa ajili ya ustawi wa wanajamii. Usimamizi tata kupita kiasi na urasimu huleta changamoto mahususi kwa washikadau wasio na rasilimali nyingi. Hii inaweza kutokeza au kusababisha ukosefu wa usawa kati ya vikundi tofauti katika jamii.



**Ushirikiano** katika ngazi ya jamii pia ni mkakati madhubuti wa kufikia mazoea ya usimamizi endelevu wa mazingira. Mfano mmoja ni usimamizi wa pamoja wa maliasili kama vile samaki, miamba ya matumbawe na mikoko.

## 4. Mifumo na sera zinazopatana na zinazotabirika huunda msingi wa kujenga ukuaji wa bluu kwa wenyeji

Sheria na sera zinahitaji kupatana na kutabirika ili wadau waweze kuelewa na kufanya marekebisho kupatana na matakwa hayo.

**Upatano** ndani ya kati ya sheria na sera tofauti ni muhimu kwa uwazi wa malengo na matokeo matokeo ambayo jamii inatanguliza

**Matokeo yanayotabirika** ni ufunguo wa utayari wa kuwekeza katika uchumi wa bluu, na hapo usalama wa umiliki na ufikiaji wa rasilimali mara nyingi ni muhimu.

Mfumo wa kitaasisi wa uchumi wa buluu unapaswa kuegemezwa katika mikakati, mipango na sera katika ngazi za juu, lakini ukuaji wa bluu **kwa wenyeji** unahitaji **kuungwa mikono kisiasa** katika ngazi ya mtaa pia.

Wakati wa kufafanua sheria na sera, ni lazima kuzingatia **muktadha** husika, hasa kwa habari ya **matokeo yoyote yasiyotarajiwa** kwa jamii kwa jumla na kwa ajili ya ukuaji wa bluu haswa.




## 5. Kanuni za mazingira zilizopatanilishwa na hali na zinazoeleweka vizuri hudumisha ukuaji wa bluu



Ukuaji wa muda mrefu wa buluu kwa wenyeji **unategemea** usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili. Mifumo ikolojia inayofanya kazi ni sharti ili ukuaji endelevu wa buluu wa uwepo. Kanuni za mazingira zinatumiwa ili kupata matumizi endelevu.

**Ufanisi** wa kanuni za mazingira na jinsi zinavyochangia ukuaji wa bluu kwa wenyeji unategemea kadiri ambayo zina **msingi wa ushahidi, kupatanishwa na muktadha na kueleweka** kwa wahusika.

Ili sera na kanuni ziwe na matokeo, mamlaka zinahitaji uwezo wa kutekeleza na kufuatilia **uzingatiaji**. Kuandaa mashirika ya wenyeji yaliyounganishwa na uchumi wa bluu na uwezo wa udhibiti na utekelezaji kunaongeza fursa za ukuaji wa bluu. Hii inaimarisha **uthabiti** wa jumuiya za pwani kwa kuwa wataelewa sababu za kanuni hizo kutumiwa na wataunga mkono umiliki wa jamii na kuwajibika kwa ajili ya rasilimali za eneo lao.

## 6. Kuunganisha hatua za kuongeza thamani na zinazofanya kazi vizuri ni muhimu kwa kuendeleza uchumi wa bluu kwa wenyeji

Biashara za bluu za wenyeji husitawi zaidi zinapounganishwa na ugavi bora, usindikaji na msururu wa masoko.

Kupata **vifaa** vilivyo bora na kwa wakati ni muhimu kwa biashara nyingi za bluu, wakati **usindikaji** kwa ujumla huongeza thamani ya bidhaa.

Uwezo wa kuelewa na kufikia **masoko** mbalimbali, yakiwemo ya kimataifa, huongeza fursa za kiuchumi. Ndivyo ilivyo katika kurekebisha bidhaa na huduma kulingana na mahitaji ya soko. Bidhaa zilizohifadhiwa vizuri zinaweza kuuzwa wakati bei ya soko iko juu. Ni muhimu kwa ukuaji wa bluu kuhakikisha si



uwazi wa masoko tu, lakini pia kujumuika kwa wauzaji na wanunuzi.

**Usaidizi unaolengwa** kwa biashara ambazo ni viunganishi muhimu vya msururu wa thamani unaohitajika kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa wenyeji, kwa sababu **msururu wa thamani inayofanya kazi vizuri** ni muhimu kwa ukuaji wa bluu kwa wenyeji.

## 7. Usimamizi bora wa taasisi zinazofanya kazi ni msingi wa ukuaji wa bluu kwa wenyeji

Ukuaji wa bluu kwa wenyeji unategemea **ubora** na **uhalali** wa taasisi na mifumo ya utawala. Utawala bora - taasisi za umma **zinazotegemewa, zisizo na ufisadi, zilizo na uwazi na uwezo** - hukuza imani ya jamii kwa taasisi zake na uhalali wao.

Mifano ya mashirika yanayotekeleza majukumu muhimu katika uchumi wa bluu ni **taasisi za umma** zinazosimamia kanuni za chakula na usalama, kurahisisha taarifa za soko, majadiliano ya mikataba na mifumo ya usafiri vijijini. Jinsi taasisi hizi zinavyosimamiwa huathiri uwezekano wa ukuaji wa bluu wa muda mrefu na endelevu kwa wenyeji.



Sifa muhimu ya utawala bora ni kuwepo kwa taratibu zinazowezesha wananchi na jamii katika ngazi zote **kuwa na sauti** katika maamuzi yanayohusu maisha yao.

## 8. Ubunifu huchochea teknolojia iliyoboreshwa na michakato bora zaidi wa uchumi wa bluu kwa wenyeji

Ubunifu huwezesha maendeleo na utumizi wa teknolojia bora zaidi katika uchumi wa bluu. Husaidia biashara za buluu kutengeneza **bidhaa** mpya, kuchunguza **masoko** mapya na **kupunguza gharama**, ikijumuisha gharama kwa mazingira na jamii.

**Uwezo** wa watu binafsi na mashirika ni muhimu kwa maendeleo na kupitishwa kwa ubunifu, na mahitaji yanahitaji kuhamasishwa. Kuimarisha uwezo wa **uvumbuzi wa mashirika ya wenyeji** huunda fursa za ukuaji wa bluu na kuimarisha uthabiti wa jumuiya za pwani. Kuwezesha **upatikanaji wa mikopo** kwa biashara ndogo ndogo za pwani kunaweza kusaidia kuimarisha uwezo huo.



Kama ilivyo kwa maendeleo ya miundombinu, ubunifu wa kiteknolojia huenda **utaleta athari mbaya zisizotarajiwa** katika suala la kuwezesha unyonyaji wa maeneo na rasilimali mpya. Kwa hivyo, uwezekano wa athari mbaya lazima zichunguzwe kwa uangalifu.

## 9. Mpangilio wa kimkakati unasaidia kuondoa vizuizi na kutayarisha njia kwa ajili ya ukuaji wa bluu kwa wenyeji.

Kupanga ni kuunda wakati ujao unayotaka. Upangaji wa kimkakati wa maeneo ya pwani na baharini huwezesha utambuzi na usimamizi ulio makini kuhusiana na **fursa na migogoro** kuhusu rasilimali na maeneo.

Michakato ya kupanga mikakati huakisi **maslahi ya kisiasa na kitaasisi** yanayoathiri maendeleo ya baadaye ya eneo husika. Kwa hiyo, kuwepo kwa mpango wa maendeleo kunatoa kiwango cha **kutabirika** na **mwongozo** kwa wawekezaji, wadau na jamii kwa uwekezaji katika uchumi wa bluu.

Ili kukuza maendeleo endelevu, ni muhimu kuzingatia **matarajio ya kiuchumi, kijamii na**



**kimazingira** katika mchakato wa kupanga mikakati. Kuwezesha jumuiya kushiriki maamuzi yanayoathiri mazingira na fursa zao ni muhimu wakati wa kupanga mkakati na usimamizi bora.

## Jinsi tulivyofanya: tafiti nne ndani ya moja

Muhtasari huu wa sera unajumlisha matokeo kutoka kwa tafiti nne zinazochunguza njia za kuondoa umaskini kwa jamii za pwani. Masomo haya yanachunguza sababu za kitaasisi na miundombinu zinazoathiri ukuaji wa bluu na maendeleo ya kijamii kwa wenyeji katika nchi zinazoendelea.

**Utafiti wa kwanza** unachanganua kesi 17 za ukuaji wa bluu wenye mafanikio katika ngazi ya jamii, kwa kuzingatia biashara ndogo za uvuvi, ufugaji wa samaki na uhifadhi (WSP, 2020). Utafiti huo unategemea mapitio ya fasihi na mahojiano ya wataalam. Inabainisha usimamizi shirikishi wa maliasili, upatikanaji wa mikopo, ujuzi wa kiufundi, misururu ya thamani yanayofanya kazi vizuri baada ya kuvuna na uwepo wa miundombinu kama vile bandari za uvuvi, uwekaji kizimbani na uhifadhi kama ufunguo wa kuwezesha ukuaji wa bluu kwa wenyeji.

**Utafiti wa pili** ni uhakiki wa mada ya fasihi ya kisayansi (Carneiro et al., 2021). Matokeo ya mapitio yanaonyesha kwamba uwezekano wa ukuaji wa bluu kwa wenyeji kuwepo ni kubwa zaidi iwapo kuna sera na mifumo ya kisheria inayoeleweka na inayotabirika, na wakati wadau wana uwezo na ujuzi wa kutosha. Taasisi za kitaifa na kimataifa na watendaji wanahitaji kurekebisha miradi na sera za uchumi wa bluu kwa mazingira ya wenyeji, kusaidia maendeleo ya misururu ya thamani inayofanya kazi vizuri na kuhakikisha kwamba kanuni za mazingira zinatekelezwa.

**Utafiti wa tatu** unatoa uchanganuzi wa maeneo na jinsi miundombinu ya msingi inavyochangia ukuaji wa bluu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi (GroundTruth, 2021). Inachunguza jamii 11 za pwani katika eneo la Bahari ya Hindi Magharibi na kuonyesha kwamba uwepo na ufikiaji wa barabara, viwanja vya ndege na umeme katika jamii za pwani huchangia ustawi wa kiuchumi. Jukumu muhimu linalotekelezwa na mpangilo wa kimkakati linakaziwa pia, ikionyesha kwamba jumuiya zilizopangwa kimkakati huwa na viwango vya juu vya ustawi wa kiuchumi na kijamii.

**Utafiti wa nne** unachunguza masomo yaliyopatikana kutokana na kuchochea ukuaji wa bluu kwa wenyeji katika jamii za pwani nchini Uswidi (Morf et al., 2021). Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi-kifani, unabainisha viwezeshaji na vizuizi pamoja na mikakati iliyotumiwa kushinda vizuizi na kuleta mafanikio. Matokeo yalionyesha matakwa na hali kadhaa ya kimsingi yaliyosaidia mipango kufaulu. Haya yanaweza kufupishwa chini ya nguzo nne za mada: uhamasishaji wa mamlaka na umiliki, uwezo na rasilimali zinazohitajika, maarifa na ujuzi husika na hatimaye, miundombinu "migumu" inayopatana na mahali.

**Zingatia kwamba** kama ilivyo na muhtasari wote, muthasari huu wa sera una vikwazo vyake. Matokeo yetu yanatokana na tafiti za sasa na za awali za hali ya ulimwengu. Kwa hiyo, vichochezi vikali vya sasa na vya siku zijazo vinaweza kuwa muhimu sana kwa ukuaji wowote wa bluu wa siku zijazo - kwa mfano viendeshaji kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, mabadiliko ya dijiti, au hali ya usalama inayobadilika.

## Mifumo ya ikolojia inayofanya kazi ni muhimu

Inafaa kusisitiza kwamba mifumo ikolojia inayofanya kazi ni sharti la maendeleo endelevu, na kwa ukuaji endelevu wa buluu wa ndani.

Kukosa kudumisha utendaji wa mfumo ikolojia kunaweza kuwa ghali sana. Na kurejesha asili inaweza kula gharama zaidi kuliko kuitunza hapo kwanza.

Maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiikolojia ni sehemu zilizounganishwa.

# Marejeleo

Carneiro, G, Göthberg, M., Hammar, L., Mattson, Y. & Sundman, M-L. (2021). Enabling local blue growth in developing countries. *[Kuwezesha ukuaji wa bluu kwa wenyeji katika nchi zinazoendelea]* Mamlaka ya Uswidi ya Usimamizi wa Bahari na Maji, Gothenburg. https://www.havochvatten.se/download/18.7eb199f517cf56701e02badd/1636447077124/rapport-2021-18-eng-enabling-local-blue-growth-in-developing-countries.pdf

GroundTruth (2021). A spatial analysis of basic infrastructure as a prerequisite for local blue growth in the Western Indian Ocean region. *[Uchambuzi wa maeneo ya miundombinu ya kimsingi kama sharti la ukuaji wa bluu wa kwa wenyeji katika eneo la Bahari ya Hindi Magharibi].* GroundTruth Water, Wetlands and Environmental Engineering. *[Maji, Ardhi Oevu na Uhandisi wa Mazingira].* https://www.havochvatten.se/download/18.764c2cb917a6c5c85b02ff55/1625582363419/rapport-spatial-analasis-of-the-role-of-basic-infrastructure.pdf

Morf, A., Sandsten, J., Prutzer, M. and Lindroth, N. (2021). Blue Economy and Coastal Development – Sharing Swedish Experiences: Conditions, challenges, enablers and lessons from seven initiatives working with local and regional collaboration for a sustainable blue economy. *[Uchumi wa Bluu na Maendeleo ya Pwani - Kushiriki Uzoefu wa Uswidi: Masharti, changamoto, viwezeshaji na masomo kutoka kwa miradi saba ya ushirikiano wa mtaa na wa wilaya kwa uchumi endelevu wa bluu].* Ripoti Na. 2021:5, Swedish Institute for the Marine Environment, Gothenburg. https://www.havochvatten.se/download/18.73c15a2717d45ecd8f0f0490/1638884857501/Blue_Economy_Sweden_Report_Final_2021-11-19.pdf

WSP (2020). Preconditions for local socio-economic development in the blue economy. *[Masharti ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wenyeji katika uchumi wa bluu].* WSP Sverige AB. https://www.havochvatten.se/download/18.1ae572bb178463a43cca4196/1617027061162/preconditions-for-local-blue-growth-with-appendix.pdf

# Kuhusu sisi

**SwAM** ni Wakala wa Uswidi wa Usimamizi wa Bahari na Maji. Tunafanya kazi kwa niaba ya bunge na serikali ya Uswidi.

**SwAM Ocean** ni ushirikiano wetu wa maendeleo. Kwa kutumia SwAM Ocean tunalenga kuongeza fursa za watu kujikwamua kutoka kwenye umaskini kwa njia ya matumizi endelevu ya bahari.

**Pamoja na washirika wetu** tunaimarisha uwezo wa kupanga kwa ajili ya wakati ujao wa bahari, kutunza na kutumia bahari - kwa furaha na manufaa ya wote.

**Inafadhiliwa na Sida**, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden.

Yaliyomo katika chapisho hili ni jukumu la waandishi na sio lazima maoni ya Sida.

Sweden Sverige

Swedish Agency for Marine and Water Management

Jipatie habari nyingi zaidi kwenye [www.havochvatten.se/swam-ocean](www.havochvatten.se/swam-ocean)



# Mambo 9 yanayowezesha ukuaji wa bluu kwa wenyeji katika nchi zinazoendelea

Muhtasari huu wa sera unajumlisha matokeo ya tafiti nne za usuli zinazochunguza hali kwa nia ya kuondoa umaskini wa jamii za pwani.

Muhtasari huo unaorodhesha mambo tisa muhimu ya kitaasisi na miundombinu yanayochochea ukuaji wa bluu kwa wenyeji kutokana na matumizi ya rasilimali za baharini katika nchi zinazoendelea.

Muhtasari huu wa sera ni matokeo ya Swam Ocean, mpango wa ushirikiano wa kimaendeleo wa kimataifa unaoendeshwa na Shirika la Uswidi la Marine na Usimamizi wa Maji.

Sweden Sverige

Swedish Agency for Marine and Water Management

Jipatie mengi zaidi kwenye www.havochvatten.se/swam-ocean